JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

TAARIFA KWA UMMA

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU UCHAGUZI NA UPANGAJI WA WANAFUNZI WA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO NA VYUO VYA UFUNDI KWA MWAKA 2017

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU UCHAGUZI NA UPANGAJI WA WANAFUNZI WA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO NA VYUO VYA UFUNDI KWA MWAKA 2017

1.0 UTANGULIZI

Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imekamilisha zoezi la uchaguzi na upangaji wa wanafunzi wa kujiunga na masomo ya Kidato cha Tano na Vyuo vya Ufundi vya Serikali kwa mwaka 2017 ambao walihitimu Kidato cha Nne mwaka 2016.

2.0 MATOKEO YA UFAULU KWA UJUMLA

Jumla ya watahiniwa wa shule **349,524** wakiwemo wasichana **178,775** sawa na asilimia **51.1** na wavulana **170,749** sawa na asilimia **48.9** walifanya mtihani wa kumaliza Kidato cha Nne mwaka 2016. Watahiniwa wa kujitegemea waliofanya mtihani huo mwaka 2016 walikuwa **47,751** wakiwemo wasichana **24,587** sawa na asilimia **51.5** na wavulana **23,164** sawa na asilimia **48.5.**

Watahiniwa waliofaulu kuanzia daraja la *kwanza* hadi la *tatu* ni **96,018** sawa na asilimia **27.60** ya watahiniwa waliofanya mtihani Tanzania Bara. Hivyo ufaulu katika mwaka **2016** uliongezeka kwa asilimia **3.15** ikilinganishwa na ufaulu wa mwaka **2015.**

3.0 TARATIBU ZA UCHAGUZI WA WANAFUNZI WA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO NA VYUO VYA UFUNDI KWA MWAKA 2017

Kwa mujibu wa mwongozo wa uchaguzi wa wanafunzi wa kujiunga na Kidato cha Tano, mwanafunzi anayeomba kuchaguliwa kuendelea na Elimu ya Sekondari ya Kidato cha Tano na Vyuo vya Ufundi hulazimika kujaza fomu ya uchaguzi ***Selform*** ambayo ndiyo fomu rasmi ya maombi ya kuchaguliwa. Kwa kutumia fomu hiyo, mwanafunzi hujaza machaguo **matano ya tahasusi (Combinations)** za masomo anayotaka kusoma na Shule anayoipenda kujiunga nayo kwa kila chaguo.

Kwa kuzingatia utaratibu huo, Mfumo wa kieletroniki wa Uchaguzi hutumika kumpanga mwanafunzi katika machaguo yake ya masomo na Shule kwa kuanzia na chaguo la kwanza hadi la tano kulingana na kiwango cha ufaulu wa mwanafunzi. Mfumo humpangia mwanafunzi chaguo la tahasusi aliyofaulu zaidi kuliko machaguo mengine.

Kwa mwaka huu 2017 Uchaguzi na upangaji wa wanafunzi wa kujiunga na Kidato cha Tano na Vyuo vya Ufundi umezingatia mwongozo wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia wa tarehe 15 Mei, 2017. Mwongozo huu unaelekeza kwamba, kigezo cha mwanafunzi kujiunga na Kidato cha Tano na Vyuo vya Ufundi ni;

i) ***AAA*** hadi **CCD** kama ***cut off point*** kwenye masomo ya tahasusi
ii) Credit 3 na pointi zisizopungua **25** kwenye Daraja,

iii) Machaguo yaliyojazwa na mwanafunzi kwenye *selform.*

iv) Nafasi zilizopo katika Shule husika

Napenda kusisitiza kwamba, vigezo hivi ndivyo vinavyotumika kwa mwanafunzi kujiunga Kidato cha Tano na Vyuo vya Ufundi kwa mwaka huu. Nia ni kuinua kiwango cha Elimu na Ujuzi kwa Elimu ya Juu Nchini.

4.0 WANAFUNZI WENYE SIFA ZA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO MWAKA 2017

Wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na kidato cha Tano mwaka **2017** wanatoka kwenye Shule za Serikali na zisizo za Serikali ambapo Shule **351** zikiwemo shule **17** mpya zimepangiwa wanafunzi.

Kati ya wanafunzi 96,018 ni wanafunzi **93,019** ndio wenye sifa za kuchaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano na Vyuo vya Ufundi kwa kuwa wamefaulu vigezo vyote vya msingi kama nilivyoainisha hapo juu. Kati ya hao, Wanafunzi **92,998** ni wa Shule *(School Candidates)* na Wanafunzi **21** walisoma chini ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima.

5.0 TAREHE YA KURIPOTI WANAFUNZI KATIKA SHULE WALIZOPANGIWA

Muhula wa kwanza kwa wanafunzi wa Kidato cha Tano kwa mwaka 2017, utaanza tarehe **17 Julai 2017** lakini kwa wanafunzi wanaongia Kidato cha Sita watafungua Shule tarehe **3/7/2017** kama ilivyokuwa

imepangwa. Kwa kuwa upangaji wa wanafunzi wanaoingia Kidato cha Tano kwa mwaka 2017 umezingatia machaguo ya wanafunzi wenyewe na nafasi zilizopo katika Shule husika, **hakutakuwa na fursa ya kufanya mabadiliko yoyote ya Shule.**

Nitumie nafasi hii, kuwaagiza **wanafunzi wote kuripoti katika Shule walizopangwa kwa wakati.** Endapo mwanafunzi atachelewa kuripoti kwa zaidi ya **siku 14 kuanzia tarehe ya kufungua Shule ,** nafasi yake itachukuliwa na wanafunzi wengine.

6.0 PONGEZI NA SHUKRANI

Napenda kuwapongeza walimu wote kwa juhudi walizozifanya katika ufundishaji na kuwezesha wanafunzi kufaulu vizuri. Hii imetokana na ushirikiano wa walimu, wazazi na walezi katika kuwapatia wanafunzi hao malezi bora.

Aidha, napenda kuwapongeza wanafunzi wote waliochaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano na Vyuo vya Ufundi, niwahimize kuendelea kuongeza bidii katika kujifunza ili waweze kufanikiwa kujiunga na mafunzo ya Elimu ya Juu baada ya kuhitimu Kidato cha Sita.

Nawashukuru sana Wadau wote wa Elimu kwa maana ya Viongozi na watendaji wa Mikoa, Wilaya na Halmashauri pamoja na wananchi kwa ujumla kwa kushiriki kikamilifu kuimarisha Miundombinu ya Shule

ikiwemo maabara na majengo mengine muhimu yaliyowezesha Shule kupokea wanafunzi wa Kidato cha Tano kwa mara ya kwanza.

Orodha ya wanafunzi waliochaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano na Vyuo vya Ufundi kwa mwaka 2017 inapatikana kwenye tovuti ya OR-TAMISEMI ya:

www.tamisemi.go.tz & www.moe.go.tz

Aidha, fomu za kujiunga na Kidato cha Tano na Vyuo vya Ufundi (joining instructions) zinapatikana kwenye shule alikopangiwa mwanafunzi na kupitia tovuti ya Ofisi ya Rais TAMISEMI ya:

www.tamisemi.go.tz

IMETOLEWA NA:

George B. Simbachawene (**Mb**)
WAZIRI WA NCHI, OR -TAMISEMI.